

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA HAMSINI NA TANO**

**21 JUNI, 2018**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA TANO – TAREHE 21 JUNI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**465. MHESHIMIWA GODBLESS JONATHAN LEMA  
(ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-  
Mishahara ya Taasisi za Umma hupangwa na Serikali. Utaratibu huo wa Serikali kupanga mishahara ya Watumishi wake huathiri pia upangaji na ukadiriaji mishahara katika Taasisi binafsi:-

Je, Serikali haioni haja ya kuboresha mishahara yake na kuzielekeza Taasisi binafsi kulipa mishahara inayoendana na hali ya maisha.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **466. MHESHIMIWA MAFTAHA ABDALLAH NACHUMA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imeanzisha utaratibu wa kutoa elimu bure na kuanza kutekeleza utaratibu huo kwa kupeleka fedha Mashuleni kidogo kidogo kulingana na idadi ya Wanafunzi husika tangu Oktoba 25, 2015:-

- (a) Je, Serikali inafahamu kwamba Shule nyingi za Msingi na za Sekondari nchini zikiwemo za Mtwara Mjini zilikuwa na madeni mengi ya Wazabuni na Steshenari;
- (b) Je, Serikali inaweza kueleza kuwa madeni hayo yatalipwa kwa utaratibu upi wakati fedha zinazotolewa ni kidogo kwa uwiano wa mwezi kwa mwaka husika.

### **467. MHESHIMIWA JUMA SELEMANI NKAMIA (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Shule za Sekondari za Farkwa na Msakwalo zilizoko Wilayani Chemba zimepandishwa hadhi kuwa za *A – level* na idadi ya Wanafunzi imeongezeka katika Shule hizo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia maji ya uhakika Shule hizo ili kuwaondolea Wanafunzi adha ya kutafuta maji.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**468. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

- Je, Serikali inaweza kueleza ni nini hasa kinachochangia uharibifu wa mazingira kwa kiwango kikubwa kati ya Sheria na usimamizi.



**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**469. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Geita – Bukoli – Kahama kwa kiwango cha lami.




### III. HOJA ZA SERIKALI:

#### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2017 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

*(Majadiliano yanaendelea)*



**DODOMA**  
**21 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**